

WIKI YA KIFARANSA: Kifaransa, lango lililo wazi Bara la Afrika na Dunia

Kauli Mbiu ya Mwaka 2017 ya Jumuiya ya Nchi Zinazoongea Kifaransa: “Ninapenda, Ninachangia”

Mkutano uliofanyika hivi karibuni wa Kilele cha Jumuiya ya Nchi Zinazoongea lugha ya Kifaransa uliofanyika huko Madagascar mnamo mwezi Novemba mwaka uliopita, ulihudhuriwa na Marais na Serikali za nchi ambazo ni wanachama wa Jumuiya ya Nchi Zinazoongea lugha ya Kifaransa au wafuatiliaji wa Jumuiya hiyo: Nchi hizo 84, inakaribia asilimia 43 ya sahari “ambayo inashirikiana kwa lugha ya Kifaransa”

Mnamo Mwaka 1970, kule Niamey, nchi 21 ziliweka Mkataba wa mapatano wa kuunda Shirikisho la utamaduni na ujuzi, ikiwa ni hatua ya mwanzo ya kile kitakachofanyika katika Jumuiya ya Nchi zinazoongea lugha ya Kifaransa.

Zaidi ya asilimia 50 ya watu ambao wanaozungumza lugha ya kifaransa kila siku ni waafrika. Nchi 27, ni nusu ya nchi zilizopo Bara la Afrika, wanashiriki kwenye Jumuiya ya Nchi zinazoongea lugha ya Kifaransa na pia kwenye Umoja wa Nchi za Afrika.

Leo hii inakadiriwa kuna takriban watu milioni 275 wanaoongea Kifaransa duniani, na sensa imekadiria watu wapatao Milioni 700 wataongea Kifaransa ifikapo mwaka 2050.

Kifaransa ni “lugha ya kiafrika” ni kati ya lugha rasmi ya Umoja wa Mataifa ambayo watu wengi wanajifunza ulimwenguni, vile vile ni lugha ya pili inayotumika katika mawasiliano kwenye vyombo vya habari na vile vile ni lugha ya tatu inayotumika katika mawasiliano ya kibiashara. Kufanya biashara na mawasiliano mbalimbali barani Afrika pamoja na ulimwengu kwa ujumla wake inaifanya lugha ya kifaransa itumike sehemu nyingi.

Ufahamu wa lugha ya Kiswahili na lugha za kigeni pamoja na Kifaransa inafungua milango ya ajira : Nchini Tanzania, katika ukanda wa Afrika Mashariki na hata nje ya mipaka ya Ukanda.

Tanzania imepakana nan nchi tatu ambazo ni washirika ya Jumuiya ya nchi zinazoongea Kifaransa: Burundi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo na Rwanda. Vile vile Tanzania imepakana na Bahari ya Hindi, iwe katika eneo la Ukanda wa Bara ya Tanzania au ukanda wa eneo la Zanzibar. Nchi nyingi za ukanda huu karibu wengi au asilimia nusu yao wanaoongea Kifaransa kwa mfano Madagascar, Mauritius, Seychelles na Umoja wa visiwa vya Comoro, zikiwa ni zile nchi ambazo ni washirika wa karibu sana.

Ujirani uliopo na nchi zinazozungumza Kifaransa, kushirikiana katika mambo mbalimbali na nchi hizo, tayari kunafanya kuwa ni kama familia moja. Takribani milioni 1,5 ya Watanzania wanaelewa Kifaransa, lugha hii ikiwa ni lugha pekee ya kigeni inayotiliwa mkazo mashuleni, ukiondoa lugha ya Kiingereza.

Katika Mkoa wa Kigoma, wanaoongea Kifaransa ni kama asilimia 6 ya watu wanaoishi mkoani hapo. Ukichukua nchi nzima, takriban asilimia 2 wanaoongea lugha hiyo. Hii inatokana na

muingiliano wa mipaka na nchi jirani – Burundi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, na vile vile uwepo wa wakimbizi kutoka nchi jirani.

Katika mazingira haya, Mabalizi wa nchi ambazo ni wanachama wa Nchi zinazozungumza Kifaransa, Mabalizi wa Heshima wa nchi mbalimbali wanaoishi Tanzania, wameunda kikundi kisicho rasmi cha mawasiliano. Shughuli mbalimbali zinazofanyika katika mashule, zikiwemo zile za kitamaduni zimekuwa zikifanyika na kutambulisha Kifaransa kama lugha inayoleta “tija”.

“Wiki ya Kifaransa”, ni wiki ambayo ni muhimu sana katika Mwaka. Kama ilivyo desturi, sherehe zinafanyika katika wiki ya tarehe 20 Machi, tarehe inayoendana na siku ya Kimataifa ya Kifaransa. Mabalizi wa nchi zinazoozongea Kifaransa wanachukua fursa hii kupendekeza ratiba yenye matukio mbalimbali ya kusherehekea siku hiyo. Shughuli mbalimbali zitafanyika bila malipo yoyote. (kama vile: kutakuwa na maonyesho mbalimbali, mashindano, michezo, maonyesho ya filamu mbalimbali za Kifaransa kutoka kila nchi inayozungumza Kifaransa, filamu zilizotafsiriwa kwa lugha ya Kiingereza, kila nchi imetoa mapendekezo kuonyesha filamu kutoka nchi zao).

Utofauti wa Kitamaduni unaleta utajiri wa lugha ya Kifaransa: lugha moja inayotumiwa na watu wengi tofauti wanaoshirikiana, wanaofahamiana na kutambuana, kupitia Umoja huu wa Kifaransa.

Jimuika nasi kuanzia tarehe 16 mpaka tarehe 26 Machi.
Nyote mnakaribishwa! A bientôt!

Mabalizi wa Nchi Zinazoozongea Kifaransa na Mabalizi wa Heshima

=====

- Mh. Bw. Paul CARTIER, Balozi wa Ubelgiji
- Mh. Bw. Ian MYLES, Balozi wa Canada
- Mh. Dr Ahamada El Badoui MOHAMED, Balozi wa Visiwa vya Comoro
- Mh. Bw. Jean-Pierre MUTAMBA, Balozi wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo
- Mh. Bw. Mohamed Yasser ELSHAWAF, Balozi wa Egypt
- Mh. Mme Malika BERAK, Balozi wa Ufaransa
- Mh. Bw. Abid BENRYANE, Balozi wa Morocco
- Mh. Bw. Eugène Segore KAYIHURA, Balozi wa Rwanda
- Mh. Mme Florence TINGUELY-MATTLI, Balozi wa Switzerland
- Mh. Mme Rima KHALAF, Balozi wa Heshima wa Senegal
- Mh. Maryvonne POOL, Balozi wa Heshima wa Ushelisheli